


## Porojo Muhimu: Toleo La Kwanza (Volume 1) (Swahili Edition)



POROJO MUHIMU, ni mfululizo wa vijitabu, vidogovidogo vitakavyokuletea mkusanyiko wa FIKRA MBALIMBALI ZA KIDUNIA, kwa lugha ya KISWAHILI, kwa kutumia mtindo wa sanaa ya mashairi.

Muhimu hasa ni WAZO, LAA baki HAMNAZO Vina Mizani MKAZO, Hebu tuache MCHEZO Shairi lenye VIGEZO, Bila WAZO ni UOZO Ubora kwetu KIKWAZO, Fikira sawa TUNAZO. Porojo Muhimu, ina lengo la kifikisha hisia na mitazamo ya jamii kutokana na maongezi ya mitaani, mitandaoni na majumbani. Hili ni toleo la kwanza. Bado mengi yako jikoni na mengine njiani. Ni porojo muhimu kwa sababu, zinafurahisha zinafikirisha, zinaelimisha na zinaweza kuwa TIBA ya magonjwa kadhaa yatokayo na MISONGO YA MAISHA. Mtu anaweza kuugua kutokana na UPWEKE, UPOTOFU WA FIKRA, NA MAMBO YA NAMNA HIYO, ambayo SABABU kubwa ni MTU kukosa MAONGEZI MAZURI TU. Kwa mfano, Porojo kama hii! TUNATUPA KISWAHILI, ROHO IWE BILA MWILI? TUNAIKOSA ASILI, UZALENDO LEO CHALI. ELIMU BORA HALILI, MHIMILI KISWAHILI. BIASHARA HASA MALI, HAZIHITAJI METHALI TUNAOGOPA KIVULI, KUHADHILI KISWAHILI SAYANSI TUNAKALILI, VIPI TUJE FIKA MBALI? TUTHAMINI KISWAHLI, ,,,,,, Unaweza kuisoma kwa haraka haraka na kuisoma siku ukiwa umechoka, matokeo yake ukatoka mkavu, kama huyu jamaa alivyosisitiza You can swim all day in the Sea of Knowledge and still come out completely dry. Most people do. ~Norman Juster Kwa hiyo, ni wakati sasa, tutambue kuwa hata Porojo nazo ZINAWEZA kuwa Mali, kwa sababu kuna ambazo zina Umuhimu katika jamii yetu. Kuthibitisha hili, hatuhitaji KUOMBA MUNGU, bali FIKIRIA DAKIKA unazotumia KUPIKA na KUPIGA POROJO, kisha KUMBUKA

KUWA MUDA NDIO nyumba,gari,chakula,malazi na kadhalika kwa sababu, MUDA NA KIASI CHA NGUVU ulichotumia,ungetumia kufanya kitu MUHIMU ZAIDI na ukapata pesa, ungenunua hivyo vitu, NA KIBAYA NA HATARI, MUDA HAURUDI TENA. Sisemi usipige POROJO, ama usisome KIJITABU HIKI, bali NASISITIZA kuwa UYAFANYE HAYO kama sehemu MUHIMU katika KUANDAA MAZINGIRA SAHIHI YA KUFANYA YALIYO MUHIMU ZAIDI KWA UBORA WA HALI YA JUU ZAIDI NA UENDELEVU. Kama unayo hayo, achana na hizi porojo,vinginevyo usikose mfululizo huu ili uyapate. Bila porojo, hatutashika mkongojo. Tutaiaga dunia tungali wabichi, na bila porojo muhimu, tutaokosa utamu, maisha kila siku yatabaki kuwa magumu na hatutaisha kulaumu.Ni wakati sasa, kila tusomalo ama tusikialo tulimengenye vizuri ili tuweze kunufaika nalo.Ni wakati wa kugeuza FIKRA za VITABIA kama UNAFIKI,UVIVU,UONGO na UBINAFSI, ambavyo vinatutafuna sana, kuwa RASILIMALI YA MSINGI. Huu ndio msingi wa harakati za vijitabu hivi. Kuchangia katika KUJENGA JAMII YENYE FIKRA ZENYE UTAMADUNI WA UBORA. Huu sio wakati wa KUSEMA Mimi mtaalamu wa FIZIKIA SIJUI SIASA, bali wakati wa mtaalamu wa Siasa kujadili MAWAZO YA KIHESABU NA MTABIBU. Si wakati wa kumshika mtoto akitangulia kuchagua nyama, bali ni wakati wa Mtoto kumkumbusha MZAZI kuiezeka NYUMBA YA BIBI yake.Si wakati wa Kusifiana kwa UJINGA, bali kusionziana kuongeza UMAKINI. Ni wakati WA AKILI,KAZI NA SAYANSI inayo MJUA MUUMBA, na si wakati wa kufurahia MAPUMZIKO BILA KUFANYA KAZI. Ni wakati wa KIASI HATA kwa UPENDO NA WEMA.POROJO MUHIMU muhimu aiseeee!.



**Porojo Muhimu: Toleo La Kwanza (Volume 1) (Swahili Edition)**

(Volume 3) (Swahili Edition) pdf by Mr Juma Ahmed of the name kwanza - Porojo Muhimu: Toleo La Kwanza (Volume 1) (Swahili. **The use of scripture in Swahili tracts by Muslims and Christians in** Porojo Muhimu: Toleo La Tatu (Volume 3) (Swahili Edition) By Mr toleo la kwanza (volume 1) - Porojo Muhimu: Toleo La Kwanza (Volume 1) (Swahili Edition). **Porojo Muhimu: Toleo La Tatu (Volume 3) (Swahili Edition) By Mr : Swahili - Poetry / Literature & Fiction: Books** Porojo Muhimu: Toleo La Tatu (Volume 3) (Swahili Edition) By Mr and origin of the name kwanza - Porojo Muhimu: Toleo La Kwanza (Volume 1) (Swahili).